East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# UTANDAWAZI NA ELIMU TUMIZI BARANI AFRIKA: HAJA YA MUSTAKABALI MPYA KWA MUJIBU WA *DUNIA YAO, MSIMU WA VIPEPEO* NA *NAKURUTO*

*Arthur K. Muhia*[1]*, Prof. Issa Mwamzandi*[2]*, Dkt. Simiyu Kisurulia*[3]

[1]Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030 – 20200, Kericho, Kenya, arthurmuhia@yahoo.com.
[2]Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030 – 20200, Kericho, Kenya, imwamzandi@yahoo.com.
[3]Chuo Kikuu cha Kabianga, S.L.P 2030 – 20200, Kericho, Kenya, kisurulia@gmail.com.

**Article history:**

*Received: 19 Aug 2019*
*Accepted: 27 Aug 2019*
*Published: 30 Aug 2019*

**Keywords**:

*Utandawazi,*
*Elimu Tumizi,*
*Afrika,*
*Dunia Yao,*
*Msimu Wa Vipepeo,*
*Nakuruto*

## IKISIRI

Makala haya ni uchanganuzi wenye madhumuni makuu ya kuchanganua uhusiano uliopo baina ya itikadi ya utandawazi na elimu tumizi barani Afrika kwa mujibu wa riwaya za *Dunia Yao* (Said A. Mohamed, 2006), *Msimu wa Vipepeo* (Kyallo Wadi Wamitila, 2009) na *Nakuruto* (Clara Momanyi, 2009). Riwaya hizi zinapendekeza kuwepo kwa mustakabali mpya unaozingatia nafasi ya maarifa asilia ya Kiafrika kwenye elimu tumizi katika kipindi cha utandawazi ili kuikomboa elimu tumizi barani Afrika dhidi ya athari hasi za utandawazi. Ukombozi huo unatarajiwa kufanikisha maendeleo barani Afrika. Uchanganuzi huu wa kimaktaba uliongozwa na nadharia ya Ujumi Mweusi. Kazi za kifasihi ambazo zinarejelewa ziliteuliwa kimaksudi kwa kuwa zinazungumzia suala la utandawazi na elimu tumizi barani Afrika. Kazi hizi zilichanganuliwa ili kuonyesha mtazamo wa kifasihi kuhusu suala tata la elimu tumizi katika jamii. Makala haya yatachangia na kuimarisha uelewaji wa matatizo yanayoikumba sera ya elimu ya Mwafrika ili aweze kutafakari kuhusu elimu tumizi yenye msingi katika maarifa asilia ya Kiafrika jambo ambalo linaweza kufanikisha maendeleo ya Mwafrika na jinsi anavyojiona.

## UTANGULIZI

Madhumuni ya makala haya ni kuchanganua uhusiano uliopo baina ya itikadi ya utandawazi na elimu tumizi barani Afrika kwa mujibu wa riwaya zilizotengwa kimakusudi. Aidha, uchanganuzi huu umedhihirisha haja ya mustakabali mpya kwenye elimu tumizi barani Afrika. Murithi (2017) anasema kuwa itikadi ni mikusanyiko ya imani, mielekeo, mitazamo na fikra zote ambazo humwongoza mwanadamu kutenda au kutekeleza anayofanya katika kipindi fulani cha wakati. Anaendelea kusema kuwa miongoni mwa vyombo vinavyotumiwa kuendeleza itikadi ni elimu ambayo imenuia kujenga ukubalifu wa itikadi husika. Katika makala haya, utandawazi ni jitihada za nchi za Ulaya zilizoendelea kuwa na dunia inayofuata itikadi moja, siasa moja, uchumi na utamaduni mmoja. Utandawazi ni mfumo unaozipendelea nchi zilizoendelea na kuzikandamiza nchi zinazoendelea barani Afrika (Mwirabua, 2014). Muppid (2004) anasema kuwa jamii nyingi ulimwenguni huchukulia utandawazi kama mfumo wa kikoloni ambao unafaa kupingwa. Katika utandawazi, mataifa ya bara Afrika yanayoendelea hupoteza uwezo wake wa kudhibiti sera za maendeleo ya

mataifa yao ikiwemo sera ya elimu. Anaendelea kusema kuwa utandawazi ni jambo ambalo haliwezekani bila ya jamii fulani kutawaliwa na zingine kwani kila jamii ina upekee wa kimwonoulimwengu na miundo yake ya kipekee.

Kimsingi, elimu ni njia ambayo hutumiwa kimakusudi na jamii kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine (Murithi, 2017). Elimu tumizi ni elimu iliyovuka mipaka ya kinadharia hivi kwamba inamwezesha mpokezi kuingiliana na kuyatawala mazingira yake kwa kujiamini. Katika makala haya, elimu hii tumizi imejengwa kwenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika. Busara na hekima ya kiwango cha juu yenye msingi na mwonoulimwengu wa Kiafrika na yenye uwezo mkubwa wa kumwezesha Mwafrika kuyadhibiti na kuyatawala mazingira yake kwa faida yake na ulimwengu kwa jumla. Elimu tumizi hupitishwa kwa watoto na wanajamii waliowazidi kiumri. Miongoni mwa majukumu ya kimsingi ya elimu hii ni kupitisha ujuzi na maarifa ya jamii husika kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kufanikisha maendeleo katika jamii husika (Wa Thiong'o, 2009; Mbiti, 1989). Hata hivyo, utandawazi unaathiri kwa njia hasi viwango vya elimu tumizi barani Afrika kwa kukandamiza maarifa asilia ya Kiafrika. Ili kuondoa ukandamizaji huo, riwaya za *Dunia Yao* ya Said A. Mohamed (2006); *Msimu wa Vipepeo* ya Kyalo Wamitila (2009;) na *Nakuruto* ya Clara Momanyi (2009) zinapendekeza kuwepo kwa mustakabali mpya unaozingatia nafasi ya maarifa asilia ya Kiafrika kwenye elimu tumizi katika kipindi cha utandawazi. Zinahimiza ukombozi wa elimu tumizi barani Afrika dhidi ya athari hasi za utandawazi.

## MSINGI WA KINADHARIA

Nadharia ya Ujumi Mweusi ndio iliyoongoza na kuthibiti uchanganuzi wa riwaya zilotengwa. Kwa mujibu wa Mokena (2017); Nkonge (2014); Wafula na Njogu (2007), nadharia ya Ujumi Mweusi iliasisiwa katika karne ya ishirini na Aime Cesaire na Leopold Senghor. Historia na maendeleo ya nadharia hii inasheheni mwonoulimwengu wa Kiafrika katika miktadha kama vile ya utumwa na ukoloni ambamo mwonoulimwengu huo hukandamizwa. Nadharia hii husisitiza umuhimu wa kurithisha mwonoulimwengu wa Kiafrika pamoja na kuuonea fahari utamaduni wa Mwafrika kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Mihimili ya nadharia ya Ujumi Mweusi ambayo imepewa umuhimu hapa ni kazi za kisanaa zikusudie kumponya Mwafrika kutokana na matatizo ya kisaikolojia na athari za ukoloni. Isitoshe, kazi za kisanaa zitumike kumwiimarisha Mwafrika, kijamii na kiuchumi kwa kuhimiza usawa wa watu wote bila kubagua. Kupitia mihimili hii miwili, elimu tumizi imesawiriwa kama chombo kikuu cha kuhifahdi na kuimarisha maarifa asilia ya Kiafrika katika kipindi cha utandawazi ili kumkomboa Mwafrika dhidi ya matatizo ya kisaikolojia yanayanomfanya ajidunishe.

## MBINU ZA UTAFITI

Makala haya ni utafiti wa kimaktaba ambao ulitumia mbinu ya uchanganuzi matini katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data ili kupata mahitimisho na mapendekezo. Mbinu hii ilituwezesha kuhusisha viwango vikubwa vya data kutoka kwenye riwaya tulizozichagua kimaksudi kwa sababu zinadhihirisha haja ya kuwepo kwa mustakabali mpya kwenye elimu tumizi barani Afrika katika kipindi cha utandawazi.

## ATHARI ZA UTANDAWAZI KWA ELIMU TUMIZI

Sehemu hii inadhihirisha athari za utandawazi kwa elimu tumizi barani Afrika kwa mujibu wa riwaya tulizozichanganua. Ili kufanikisha hili, tumeigawa katika mada ndogo zifuatazo: dhana potofu kuhusu elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika, kupuuzwa kwa elimu tumizi katika ukuzaji wa uongofu na jukumu la wazazi kutwaliwa na vyombo vya kiteknohama.

### Dhana Potofu Kuhusu Elimu Tumizi Yenye Msingi wa Maarifa Asilia ya Kiafrika

Kwa mujibu wa riwaya tulizozichanganua, elimu tumizi imejengwa kwenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika. Hata hivyo, utandawazi umeathiri kwa njia hasi elimu tumizi kwa kuendeleza dhana potofu kuhusu elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika kama tulivyodhihirisha kwenye sehemu ifuatayo.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, Mhusika Julia anasikitika kuwa, bintiye, Ndumi hana hamu ya kwenda kwenye mazoezi ya 'gymnastics na skating' ambayo kimsingi ni mazoezi ya michezo ya kuteleza kwenye barafu. Julia anaamini kuwa katika ulimwengu wa kiutandawazi michezo ya aina hii inafaa kumtayarisha Ndumi kwa ajili ya maisha yake ya baadaye atakapoenda kusomea Ulaya ambako Julia anaamini kuna elimu tumizi ya kiwango cha juu na inayochochea uvumbuzi ikilinganishwa na elimu inayozingatia maarifa asilia ya Kiafrika. Madai haya ya Julia yanaungwa mkono na waziri Mkurutu katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* (kur. 57-58), alipokuwa ameabiri motaboti kwenda kisiwani huku akiona haya abiria wengine wasigundue ndiye waziri wa utalii ambaye ameshindwa kuyashughulikia maeneo ambayo yanailetea nchi pato kubwa la kigeni. Anamtazama kwa makini abiria mmoja mwanamume Mzungu; kwa kumwangalia, waziri Mkurutu anakumbuka picha za Wazungu walioitwa wavumbuzi katika vitabu vya Historia walivyotumia shuleni zamani. Vitabu vya historia vya aina hii walivyovitumia akina Mkurutu shuleni vinachangia kuwepo kwa elimu inayomkumbusha Mwafrika kadhia ya ukoloni zaidi kuliko kuwepo kwa maarifa asilia ya Kiafrika ambayo humtofautisha Mwafrika na mtu mwingine ulimwenguni.

Pia katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, dhana potofu kuhusu elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika inasababisha kudharauliwa kwa vyuo vikuu vya Kiafrika na kutukuzwa kwa vile vya ughaibuni. Watoto wa Waafrika wa tabaka la juu wanaishia kujiunga na vyuo vikuu vya Uingereza, Marekani, Australia na wachache Kanada baada ya kusomea katika shule za kibinafsi zenye kufuata mifumo ya elimu ya nchi hizo za ughaibuni. Hali hii inasababisha kudharauliwa kwa vyuo vikuu vilivyoko barani Afrika kwa kusawiriwa kama ambavyo haviwezi kuibua uvumbuzi unaoweza kumwezesha Mwafrika kuyatawala mazingira yake.

Tukirejelea riwaya ya *Nakuruto*, dhana potofu kuhusu elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika inamdhalilisha Mwafrika kiasi cha kumfanya aamini kuwa hawezi kuwa mvumbuzi wa kitu chochote cha manufaa. Msimulizi anaeleza kuwa:

> *"…nikisema hakuna jema liloletwa na watu hawa nitakuwa ninadanganya. Wanguzu hao waliwafundisha wanakijiji maarifa na taaluma katika mambo mengi. Wengine hata waliweza kuzuru nchi yao ili kuhitimu katika taaluma mbalimbali. Lakini jambo linalotukereketa zaidi ni jinsi wanavyowapuuza watoto wetu waliosoma…wewe fikiria, hata matarishi wanatoka kwao kuja kuajiriwa hapa…Tokea mameneja, wakurungenzi, wahandisi, wasanifu mijengo, makarani hata wafagiaji …wote wanatoka ughaibuni. Je, kwetu hakuna matarishi, hakuna wajuao ukarani au hata ufagiaji?...sisi tumesalia kuwa maboi tu majumbani mwao, wapagazi wa kubeba shehena za bidhaa zao, wachimbaji madini kwenye mgodi ulio katika ardhi yetu na matopasi tu."* (Nakuruto, kur. 59-61)

Hapa Mwafrika amesawiriwa kama asiye na uwezo wa kutekeleza majukumu mbalimbali yanayohitaji ujuzi wa kiwango chochote hata cha chini. Wao wanasalia tu kuwa watumwa katika shughuli nyepesi zisizofikirisha sana. Hii ni kasumba ya kiutandawazi inayolenga kukandamiza maarifa asilia ya Kiafrika.

Pia katika riwaya hii ya *Nakuruto* (uk. 131), tunakumbana na jazanda ya ujenzi wa ngazi ya kumwezesha Mwafrika kuyafikia maendeleo katika ulimwengu ulioathirika na utandawazi. Baada ya ujenzi wa muda, ujenzi unatatizwa na ukungu mzito. Ili kukabili ukungu huu, Waafrika wanashauriwa na Bw. Bullyson (mjumbe wa utandawazi) kuwa waagize kurunzi kutoka kwao ughaibuni kwa njia ya mkopo wenye masharti magumu kwa Mwafrika. Hii ni kanuni ya kiutandawazi. Kurunzi hii inapoagizwa msimamizi wake anakuwa ni Bw. Bullyson mwenyewe na ndiye anayefaa kuwapeleka wajenzi huko juu ya ngazi. Jazanda hii inadhihirisha jinsi Mwafrika ametawaliwa na kukandamizwa kifikra na utandawazi. Anaaminishwa kuwa hana uwezo wa kuvumbua kama wenzake wa ughaibuni ambao wanamruhusu afaidi uvumbuzi wao kwa mikopo na misaada yenye masharti. Pia anaaminishwa kwamba hana uwezo wa kutumia vyombo vilivyovumbuliwa ughaibuni pasipo msaada wa watu kutoka huko ughaibuni. Hali hii ndio inayosababisha taasisi za elimu kukosa imani na elimu yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika

hivi kwamba taratibu za mitaala ya elimu barani Afrika zinalenga tu kufundisha kwa minajili ya kuufikia na kuuiga utandawazi.

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* athari za utandawazi kwa elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika zinadhihirishwa kupitia kwa jazanda ifuatayo:

> *"Sote tumekumbwa na ugonjwa wa ajabu unaotuangusha kwenye maweko ya chini kabisa mwanadamu awezako kuangukia. Ajabu! Sisi ni watu tuliokuwa zamani imara, watundu, wadadisi, watetezi wa nafsi zetu, wapigania heshima ya nchi yetu. Watu tuliosimama kidete kwa miguu yetu isiyochoka-kwa fahari na kujisifu…mimi lakini najaribu sana kujikinga na ugonjwa huu! Ugonjwa ahasi! Ugonjwa wa kujidunisha mwenyewe kwa mwenyewe…ugonjwa wa aibu na fedheha." (Dunia Yao*, kur. 2-3)

Maradhi yanayorejelewa hapa ni ufumbaji wa kijazanda kuhusu kukandamizwa kwa elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika na utandawazi. Suluhisho au kinga yake ni ukombozi wa maarifa asilia ya Kiafrika kwa lengo la kuhakikisha kuwepo kwa elimu tumizi ili Mwafrika arejee katika hali yake ya awali alipokuwa na uhuru kamili wa kuyatawala mazingira yake.

Uchanganuzi wa riwaya tulizozichagua umebaini kuwa kasumba za kiutandawazi zimeibua dhana potofu yenye kudunisha nafasi ya elimu tumizi katika maisha ya Mwafrika. Sehemu ifuatayo inafafanua namna utandawazi umesababisha kupuuzwa kwa elimu tumizi katika jukumu la kukuza uongofu miongoni mwa wanajamii.

## Kupuuzwa kwa Elimu Tumizi Katika Ukuzaji wa Uongofu

Elimu tumizi yenye kuzingatia maarifa asilia ya Kiafrika huwafundisha watoto kuepukana na dhambi na kuwa na mwenendo mwema, hivyo kukuza uongofu. Hili hufanikishwa kupitia kwa masimulizi. Uongofu huwaepusha wanajamii na kiburi ambacho kinaweza kusababisha kuporomoka kwa ufanisi maishani (Nangoli, 2002). Madai haya yameangaziwa katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* (uk. 2) pale ambapo mhusika Julia anakumbuka maneno yaliyosemwa na watu kijijini alimokulia akiwa mchanga kwamba mtu akionyesha kiburi kutokana na ufanisi, miungu wanaweza kumporomosha. Hapa inabainika kuwa kabla ya utandawazi, katika jamii alimokulia mhusika Julia, ilikuwepo elimu tumizi iliyowaongoa wanajamii ili waepuke kiburi. Hali hii ni tofauti katika kipindi cha utandawazi ambacho Julia ni mzazi na amepuuza na kudharaua masimulizi ya shirikina ambayo ni sehemu ya elimu tumizi.

Julia hamsimulii wala kumweleza mwanawe Ndumi kuhusu maarifa asilia ya Kiafrika aliyofundishwa akiwa mchanga huko kijijini alimokulia kuhusu uwezo wa miungu kumporomosha mtu mwenye kiburi. Badala yake anadai kuwa katika ulimwengu huu wa kiutandawazi uwezo wa miungu ni itikadi iliyopitwa na wakati. Hili linamfanya Ndumi akose kufaidi elimu tumizi iliyojikita katika msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika na kudhamiria kujenga na kuimarisha uongofu miongoni mwa watoto.

Riwaya ya *Dunia Yao* inafafanua namna utandawazi umeathiri elimu inayolenga ukuzaji wa uongofu kwa kutueleza kuwa katika kipindi hiki cha utandawazi utaratibu wa uongofu kupitishwa kwa watoto na wanajamii waliowazidi kiumri umepuuzwa. Matokeo ya upuuzaji wa utaratibu huu ni watoto kukosa kuwaheshimu wazazi. Haya yanadhihirika kupitia kwa mhusika Yungi ambaye anamkabili Ndi, babake, na kumfokea kwa nia ya kumfahamisha kuwa utaratibu wa elimu tumizi inayozingatia uongofu umepitwa na wakati kupitia maneno yafuatayo:

> *"Wakati umebadilika. Watoto kuanzia sasa watawaendesha wazee wao…hakuna cha mila wala desturi fungua macho…majirani wote wanawaachia watoto wao wa kike na wa kiume wafanye wanavyopenda siku hizi. Wewe bado unang'ang'ania ukale. Wewe bado unataka kukamata na kudhibiti. Unataka uongozi usiouweza. Huwezi tena kutuendesha!"* (*Dunia Yao*, kur. 25-26)

Maneno haya ya Yungi ni ithibati ya jinsi utandawazi umeathiri utaratibu wa kuwa watoto wanafaa kuzingatia maelekezo ya wazazi na wanajamii waliowazidi kiumri ili wafanikiwe katika kuyakabili maisha. Yungi anaona utaratibu huo kama uliopitwa na wakati. Mtazamo huu wa

Yungi unamfanya Ndi asononeke ndani kwa ndani na kutamani kumjibu Yungi kama hatua ya kumwokoa kutokana na njia mbaya iliyomwelekea. Kupitia unzungumzaji nafsia, Ndi anasema:

> *"...ningepata wapi kauli ya kujibu?...mimi si baba ninayeng'ang'ania ukale…lakini nilijua ni vigumu kwa vijana hawa kufahamu hatari iliyomo ndani ya usasa wanaoutaka. Na wao hawalaumiki, ukitazama kasi ya mambo ya usasa na utandawazi inavyosonga*" (*Dunia Yao,* kur. 25-26)

Hapa Ndi anahuzunika kwa kujihesabu kama mzazi aliyeshindwa kutekeleza wajibu wake wa kumhakikishia mtoto wake elimu tumizi yenye kuzingatia uongofu. Hata hivyo, anakumbuka kwamba Yungi anaishi katika kipindi cha utandawazi ambapo vijana ndio wanaodhibiti maisha yao wenyewe bila kufahamu hatari iliyomo katika kuishi maisha yasiyozingatia ukuzaji wa uongofu. Kwa hivyo Ndi hajashindwa kuzingatia uongofu kwenye malezi na elimu ya mwanawe kwa sababu ya kukosa ujuzi unaohitajika ila ni kwa sababu ya athari za utandawazi zinazomfanya Mwafrika ajidunishe kama inavyopambanua nadharia ya Ujumi Mweusi katika makala haya.

Katika riwaya ya *Nakuruto*, hali ya utandawazi kuathiri ukuzaji wa uongofu si tofauti. Tunakumbana na vijana wanaojibizana na wazee wenye umri wa wazazi wao na kuwafedhehesha. Mzee mmoja anapoeleza walivyoukaribisha utandawazi barani Afrika kwa kutofahamu athari zake hasi kwa nia ya kuitahadharisha jamii dhidi ya utandawazi, vijana hawampi nafasi ahitimishe maelezo yake. Wanamchachawiza kwa kumkejeli kuwa ni kibaraka cha wakoloni mamboleo. Vijana hawa wanafanana kitabia na mhusika Yungi katika riwaya ya *Dunia Yao*. Wangekuwa waongofu wangempa nafasi mzee huyu ahitimishe maelezo yake kama anavyowashauri mhusika mkuu, Nakuruto, (*Nakuruto,* uk. 42).

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, shirika lenye msingi wa kiutandawazi la 'Global Foundation' ambalo lilikuwa na mawakala katika mataifa ya Ulaya linawatia watoto wa kike kwenye ukahaba kwa madai ya kuwapa nafasi za elimu bora. Hili linaathri elimu ya mtoto msichana inayoshirikisha ukuzaji wa uongofu. Riwaya hii inatupa mfano wa shirika lenye umbo la kiutandawazi linalojulikana kama Bordello Agencies. Tawi la shirika hili katika mji wa Frankfurt Ujerumani linawachukua watoto wa kike kutoka mataifa ya Kiafrika, wengine wenye umri wa chini ya miaka kumi na mitatu, na kuwazongomeza kwenye biashara ya ukahaba kama anavyogundua baadaye mwanahabari shupavu, Kalulu (*Msimu wa Vipepeo*, kur. 211-212). Kwa mujibu wa nadharia ya Ujumi Mweusi, watoto hawa Waafrika wanashawishika kujiunga na shirika hili kutokana matatizo ya kisaikolojia yanayofanya waamini kuwa wakienda Ulaya watafanikiwa maishani pasipo kutathmini wanachoenda kufanya.

Maelezo katika sehemu hii kuhusu namna utandawazi umeathiri kwa njia hasi ukuzaji wa uongofu kama sehemu ya elimu tumizi inazozingatia maarifa asilia ya Kiafrika yamebaini kuwa; kwanza baadhi ya wazazi wamechangia hali hii kwa kupuuza elimu tumizi inayozingatia uongofu. Hii ni kutokana na dhana kuwa elimu ya aina hiyo imepitwa na wakati. Pili, baadhi ya watoto wenyewe hasa wenye umri wa ujana wamekengeushwa na utandawazi hivyo kukosa kuwaheshimu wazazi ambao wanatarajiwa wawaelekeza kwenye uongofu. Katika sehemu ifuatayo tunatoa maelezo kuhusu jukumu la wazazi kukuza uongofu kuchukuliwa na vyombo vya kiteknolojia kama sehemu ya athari za utandawazi kwa malezi na elimu.

### Jukumu la Wazazi Kutwaliwa na Vyombo vya Kiteknohama

Vyombo vya kiteknohama ni vyombo vya kisasa vya teknolojia ya habari na mawasiliano vilivyoenea kote ulimwengu karne hii ya utandawazi. Riwaya tulizozichanganua zaonyesha kuwa badala ya wazazi kulitelekeza jukumu lao la kufundisha elimu tumizi inayonuia kukuza uongofu miongoni mwa watoto, jukumu hili limetwaliwa na vyombo vya kiteknohama. Katika riwaya ya *Nakuruto*, mhusika Nakuruto anashuhudia wanajamii wakitekwa na shughuli ya ujenzi wa ngazi ya kuufikia utandawazi kiasi cha kusahau jukumu la kufanikisha malezi yanayozingatia elimu tumizi kwa watoto wao. Matokeo yake ni kuibuka kwa kizazi kipya cha watoto waliopotoka kutokana na malezi dhaifu yasiyozingatia elimu tumizi yenye maadili na uongofu kama anavyoeleza msimulizi kupitia usemi huu:

> *"Watoto walikuwa kama kondoo waliokosa wachungaji. Walezi waliacha majukumu ya kuwalea wakaingia kwenye mbio za kuisaka harufu ya nta*" (*Nakuruto*, uk. 140)

Usemi huu unatujengea taswira ya watoto ambao wazazi wao wanajishughulisha na jitihada za kuishi maisha ya kutafuta pesa bila kujali majukumu yao katika malezi. Hapa pana utundikaji ambao unatuhitaji kujiuliza nani ambaye anatekeleza jukumu hili wasilolitelekeza wazazi. Jukumu la wazazi la kuhakikisha kuwa malezi yamejengeka katika msingi wa elimu tumizi katika kipindi hiki cha utandawazi limeachiwa vyombo vya kiteknohama hasa runinga kwa mujibu wa riwaya ya *Dunia Yao*. Msimulizi anadhihirisha madai haya kwa kusema kuwa:

> "*Tazama taathira ya vyombo vya habari na mawasiliano vinavyosambaza uhalifu, uwongo na unafiki…ukatili unavunja hisia ya vijana. Hisia ya maisha inazidi kupotea. Lakini nani anayejali?...binadamu ana uhuru wake. Binadamu ana uwezo wa kupima baya na zuri. Si ukatili. Si silaha zinazomfanya kijana anyanyue bunduki kumwua mama, baba na ndugu yake. Kisha atoke nje kuua wapitanjia na mwisho ajimalize mwenyewe. La, si michezo ya kikatili wanayoiona vijana kwenye video, DVD na sinema. Si bunduki, si silaha zinazoundwa na kuuzwa. Labda polisi tu hawafanyi kazi zao. Au hakuna mafunzo kwa vijana ndani ya koo zao. Mafunzo ya kutofautisha ukweli na uwongo! Huu ndio upeo wa dunia ya leo. Dunia Yao!"* (*Dunia Yao*, uk. 49)

Hapa msimulizi anafafanua athari hasi ya vyombo vya habari na mawasiliano kwa malezi na elimu kwa kutumia kejeli kuwa matatizo yanayowakumba vijana kama yanavyofafanuliwa kwenye dondoo huenda yamesababishwa na polisi kutofanya kazi yao. Hatimaye linatolewa jibu thabiti kuwa kiini cha matatizo yenyewe ni ukosefu wa mafunzo kwa vijana ndani ya koo zao ili waongoke kiasi cha kuweza kutofautisha ukweli na uwongo. Badala yake nafasi ya mafunzo haya imetwaliwa na michezo ya kikatili wanayoitazama vijana kupitia vyombo vya kiteknohama kama vile video, DVD na sinema. Matokeo yake yanakuwa maangamizi ya jamii nzima kutoka wazazi hadi watoto jambo ambalo bila shaka litasababisha kukandamizwa na kudidimia kwa elimu tumizi yenye msingi katika maarifa asilia ya Kiafrika.

Sehemu hii imefafanua athari hasi za kuviachia vyombo vya kiteknohama jukumu la wazazi katika malezi na elimu tumizi. Kilele chake ni kuangamia kwa jamii inayoyamiliki elimu tumizi na bila shaka jamii ikingamia elimu tumizi haitasalimika. Baada ya kutoa maelezo kuhusiana na athari za utandawazi kwa elimu tumizi, katika sehemu ifuatayo tumedhihirisha jinsi riwaya tulizozichanganua zimesisitiza haja ya mustakabali mpya kwenye elimu tumizi barani Afrika.

## Ukombozi wa Elimu Tumizi Dhidi ya Athari za Utandawazi

Sehemu hii inaangazia ukombozi wa elimu tumizi dhidi ya utandawazi kwa mujibu wa riwaya tulizozichanganua. Ili kufanikisha hili, tumeigawa katika mada ndogo zifuatazo: mustakabali mpya kwenye elimu tumizi barani Afrika, kuhimiza elimu tumizi katika ukuzaji wa uongofu na jukumu la wazazi kutiliwa nguvu na vyombo vya kiteknohama.

### Mustakabali Mpya Kwenye Elimu Tumizi Barani Afrika

Katika sehemu hii tumefafanua ukombozi wa maarifa asilia kama suluhisho la dhana potofu kuhusu elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika. Dhana hii potofu imesababisha matatizo ya kisaikolojia kwa Mwafrika kama tulivyodhihirisha katika sehemu iliyotangulia. Ukombozi huu unaungwa mkono na mhimili wa kwanza wa nadharia ya utafiti katika makala haya ambao unasema kwamba kazi za sanaa zikusudie kumponya Mwafrika kutokana na matatizo ya kisaikolojia, utandawazi na udunishwaji kwa jumla. Hili linafanikishwa kwa riwaya tulizozichanganua kusawiri maarifa asilia ya Kiafrika kama msingi wa elimu tumizi. Elimu iliyovuka mipaka ya kinadharia hivi kwamba inamwezesha mpokezi kuingiliana na kuyatawala mazingira yake kwa kujiamini.

Katika Riwaya ya *Dunia Yao*, msimulizi anasema kuwa ili kufanikiwa kwa elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika lazima Mwafrika ajipeleke ndani ya nafsi yake kuzungumza na akili

zake kwa maana ya kuichangamkia elimu tumizi kama inavyodhihirika kwenye dondoo ifuatayo:

> *"…mimi lakini najaribu sana kujikinga na ugonjwa huu! Ugonjwa ahasi! Ugonjwa wa kujidunisha mwenyewe kwa mwenyewe… ugonjwa wa aibu na fedheha …Hii ndwele mpya lazima nijikinge nayo …ni ndwele ya aibu ya nafsi yangu. Kinga yake kubwa, nahisi ni kujipeleka ndani ya nafsi yangu kuzungumza na akili yangu. Niieleze ifahamu sababu na matokeo ya jiwe moja zito lililokuja kuongeza uzani na kunivunja uti-wa-mgongo na kufikia hata kuuvunja uume wangu*." *(Dunia Yao,* uk. 2-3)

Kujipeleka ndani ya nafsi ni ufumbaji wa kijazanda unaorejelea elimu tumizi itakayomfaa Mwafrika katika kuziponya akili zake kutokana na kukandamizwa na utandawazi uliommaliza nguvu pamoja na kizazi chake cha usoni jambo linalosawiriwa kupitia kwa taashira ya kumvunja uti wa mgongo na uume wake. Mtu aliyevunjwa viungo hivi viwili vya mwili hatarajiwi kuwa na kizazi. Kizazi kikikosa mrithi wa elimu tumizi ili airithishe kizazi cha baadaye atakosa na bila shaka elimu hiyo itaangamia. Kupitia kwa usemi tuliounukuu hapo juu, riwaya ya *Dunia Yao* inasema kwamba ili vizazi vinavyofaa kurithishwa viwepo, lazima kwanza kuwepo na mustakabali mpya wa kuimarisha elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika.

Tukirejelea warsha ya utalii katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, tunakumbana na wanawarsha, akiwemo mhusika Mkurutu ambaye ni waziri wa utalii, wakijadili umuhimu wa kuanzishwa kwa chuo cha kutoa elimu tumizi. Chuo hiki kinatarajiwa kushughulikia sayansi ya bahari katika kisiwa cha Kisiwandeo mjini Gongwa kama juhudi za kuyakomboa maarifa asilia ya Kiafrika kama inavyodhihirika katika dondoo ifuatayo:

> *"…Kisiwa cha Kisiwandeo- kisiwa ambacho alipokuwa shuleni waliambiwa kilikuwa makao adhimu ya mamwinyi wa Kiarabu; kisiwa ambacho mwalimu wao mmoja alidai ndiko kulikokuwa na chuo kikuu cha kwanza nchini. Kisiwa ambako ilidaiwa kuwa zamani watu wa kutokea Uchina walifika na hata kuacha vizalia vyao humo. Alitaka kuyaona maendeleo ya kisiwa hicho tangu enzi zao…*" (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 52)

Uanzishaji wa chuo ulikuwa tayari umeidhinishwa miaka sita kabla ya warsha hii lakini waziri wa utalii wa wakati huo akapinga kwa kuwa hakuwa mwenyeji wa eneo hilo. Alipendekeza kijengwe eneo lake lakini hili halikutekelezwa. Hii ni jazanda ya kiukombozi kuhusu elimu tumizi ambapo waziri huyu wa utalii alitaka chuo kijengwe kwenye eneo ambalo halina utajiri wa maarifa asilia ya Kiafrika kihistoria. Ukombozi unadhihirika kwa kucheleweshwa kwa kujengwa kwa chuo hadi makubaliano ya sehemu ya ujenzi yapatikane. Sababu kuu ya eneo la Gongwa kupendekezwa na Mkurutu liwe makao ya chuo kinachopendekezwa ni kuwepo kwa kisiwa cha kihistoria katika eneo hili. Makala haya yanachukulia kuwa kisiwa hiki kina utajiri mkubwa wa maarifa asilia ya Kiafrika yanayoweza kuimarisha elimu tumizi kutokana na historia yake ndefu.

Maelezo hayo kuhusu mapendekezo ya kuanzishwa kwa chuo barani Afrika katika msingi wa elimu tumizi yanaungwa mkono na mhusika Ndumi katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ambaye anaamini kuwa ili upokee elimu tumizi inayokuwezesha kuwa mvumbuzi, sio lazima uende kusomea Ulaya kama wanavyoamini Mkurutu na Julia, wazazi wake. Hili linadhihirika anapochukizwa na himizo la Julia kuwa ajifundishe michezo inayoambatana na mazingira ya Ulaya kama vile utelezaji juu ya barafu kama njia ya kujitayarisha kwenda kusomea Ulaya alikoamini Julia kuna elimu inayochochea uvumbuzi. Kwa upande wake Ndumi, anaonyesha kupendezwa na elimu inayopatikana kwenye vyuo vya Kiafrika kwa kuwaenzi wanafunzi wa vyuo vinavyotoa elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika kama vile Mtanu anayesomea katika chuo kikuu cha Kitambasire. Elimu aliyoipokea Mtanu katika chuo kikuu cha Kitambasire, inamwezesha kuwa na maarifa ya kuchangia katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii yake kwa mfano kuhimiza lishe bora ili kuimarisha afya kwa kuwafundisha wanajamii kwa ustadi uhusiano uliopo baina ya lishe na magonjwa.

Mwanafunzi mwingine anayesomea katika chuo cha Kiafrika na ambaye Ndumi anamuenzi ni binamu yake, Kalulu. Licha ya kuwa Kalulu

amesomea taaluma ya uanahabari katika chuo cha Kiafrika, anakuwa mwanahabari shupavu. Kupitia kwa Kanda, habari za watoto wa kike kuchukuliwa Ulaya na shirika la Globle Foundation kwa kusingizia wanaenda kusoma ilhali wanaenda kushirikishwa kwenye shughuli za ukahaba zinachipuka. Kanda pia anafichua uchafuzi wa bahari na kampuni moja ya kusafirisha mafuta akiwa na nia ya kuhakikisha uhifadhi wa mazingira. Kwa upande mwingine, riwaya inafika mwisho pasipo kukumbana na mchango wowote unaokusudia kuiletea jamii maendeleo kutoka kwa wanafunzi waliosomea vyuo vya ughaibuni vilivyotukuka kiutandawazi. Wakishafika ughaibuni hatuwasikii tena. Ulinganuzi huu wa kuwaonyesha waliosoma ughaibuni kama wasio na mchango thabiti katika maendeleo ya jamii wakilinganishwa na waliosoma katika vyuo vya Kiafrika ni mkakati wa kiukombozi unaohimiza haja ya mustakabali mpya kwenye elimu tumizi barani Afrika.

Tukirejelea riwaya ya *Nakuruto*, juhudi za kuyakomboa maarifa asilia ya Kiafrika ili yawe msingi wa elimu tumizi zinadhihirika kupitia mazungumzo ya vijana Waafrika kuhusu elimu tumizi kwa Mwafrika. Mazungumzo haya yanaongozwa na mhusika Maridhia kama yanavyodhihirika kwenye dondoo ifuatayo:

> "*Hata vipanya tunaviendesha sawasawa. Tunasanidi program tunazoagiza kutoka ughaibuni na tunajua mengi yanayotendeka katika sayari hii…jamii ya Quick Buck hujali maslahi yao tu. Hata tukifaulu kuunda program zetu wenyewe huenda wakazitupia virusi. Kwanza hawatakubali sisi tumiliki nta au hata kutengeneza yetu wenyewe. Hata tukajiundia kinga virusi, watahakikisha wameharibu programu…tujiulize kwa nini uvumbuzi unapotokea vijijini hauthaminiwi lakini uvumbuzi wa aina iyo hiyo unapotokea ughaibuni tunauheshimu na kuuenzi?...tutumie ujuzi wetu kwa kujiheshimu…tusikubali kuwa sisi wenyewe hatuna wataalamu wa kutuongoza au kuamini kuwa kilicho kizuri lazima kitoke kwa kina Quick Buck*." (*Nakuruto*, uk. 143-145)

Dondoo hii ni jazanda inayosema kuwa hata Mwafrika anaweza kuwa mvumbuzi wa nyenzo zinazomwezesha kukabiliana na maisha katika kipindi cha utandawazi akitumia maarifa asilia ya Kiafrika. Tatizo ni kuwa Mwafrika ameaminishwa na utandawazi kuwa uvumbuzi wake ni dhaifu ila uvumbuzi sawa na ule wake ukitokea ughaibuni anafaa kuukumbatia. Dondoo hii imekusudia kwanza, kumponya Mwafrika kutokana na matatizo ya kisaikolojia ya kudunishwa kwa uvumbuzi. Pili, imekusudia kutetea dhana kwamba elimu tumizi yenye msingi katika maarifa asilia ya Kiafrika ina nafasi muhimu katika ulimwengu wa kiutandawazi. Madai haya yanalingana na mhimili wa kwanza na wa pili wa nadharia ya utafiti katika Makala haya.

## Kuhimiza Elimu Tumizi Katika Ukuzaji wa Uongofu

Uhimizaji wa elimu tumizi kama mkakati wa kukuza uongofu unaanza kwa utundikaji wa kuwepo au kutokuwepo kwa elimu tumizi kupitia kwa mhusika mkuu Ndi katika riwaya ya *Dunia Yao.* Ndi anasema hivi kupitia uzungumzaji nafsi:

> *"Labda nipo. Pengine sipo! Tofauti gani? Ndiyo, moyo bado unatuta. Hii labda ndiyo ishara pekee iliyobaki…afadhali uamke. Ilinijia tu niinuke hatimaye. Niinuke kusema na wahusika wangu, kwani sikuwa na mwingine wa kusema naye katika hii dunia ndogo, ndani ya kijichumba hiki kama jela, humu nilimojikomelea mimi mwenyewe kwa hiari yangu. Kabisa sikutarajia kama ningefika chini hivi…kinga yake kubwa ni kujipeleka ndani ya nafsi kuzungumza na akili…" (Dunia Yao,* uk. 1-3).

Ndi anafananisha dukuduku hili la kuwepo au kutokuwepo na ugonjwa wa aibu na wa kujidunisha mwenyewe kwa mwenyewe. Utundikaji huu unaeleza kwamba kuna haja ya elimu tumizi kukombolewa kutoka kwa kukandamizwa na utandawazi. Ikishakombolewa, elimu hii inatarajiwa kupata nafasi katika maisha ya wahifadhi wake ambao ni Waafrika ili wakome kujidharau na wakuze uongofu utakaowawezesha kujithamini. Hili linamfanya asiwe na budi kuanza harakati za ukombozi wa elimu tumizi dhidi ya utandawazi.

Riwaya ya *Dunia Yao* inaendelea kufafanua ukombozi wa elimu tumizi kwa kutumia jazanda ya

mshumaa kudhihirisha mchakato wa ukuzaji wa uongofu.

> *"…kijishumaa kidunya kilijipiga kofi chenyewe, kikajizima kukamilisha giza…humu gizani…kijitambi chake kilihangaika na hatimaye…pua yangu ikajaa harufu ya mshumaa uliokuwa ukizimika. Hapo hapo nikageuka kipofu na kuanza kupapasa dunia nisiyoiona, lakini ninayoifahamu vyema. Nilitomasa njia kuelekea pale nilipodhani palikuwa na swichi ya taa. Parrr…mkono ulikwenda kwa mazinduzi. Kujaribu tu si kwa tamaa ya kuwaka taa. Parrr…mkono ukaparika…swichi hii hatimaye. Tat, swichi ikatatia. Mwangaza haukuja lakini. Aaa, sikustaajabu…nilibanduka hapo. Nikaanza kwenda. Kwanza nikijaribu kuihisi na kuipapasa njia kifikra…katika dunia hii, lazima ujue namna ya kutumia chochote haba kinachobaki. Papasi nyingine tena- mshumaa mpya ukaingia ganjani…mshumaa usingewaka ningebaki kukumbatiwa na giza humu gerezani. Kwa bahati nzuri lakini, kilimi cha mshumaa kilianza kufufuka na kuimarika. Hatimaye kilijifaragua, kikaambuza mwanga wa kutosha" (Dunia Yao, uk. 5*-6)

Msimulizi anasema kuwa kama mshumaa ambao unaelekea kuzimika, elimu tumizi iliyokandamizwa na utandawazi usingewaka angebaki kukumbatiwa na giza gerezani ambako chombo cha kitandawazi (swichi), kimeshindwa kumtatulia tatizo lake. Gereza hapa ni jazanda ya ulimwengu unaotawaliwa na utandawazi ambao unawakilishwa na giza. Hatimaye kilimi cha mshumaa kinaanza kufufuka na kuimarika. Kinajifaragua na kuangaza kwa mwanga wa kutosha. Mchakato kinaopitia kilimi cha mshumaa ili kutoa mwanga ni harakati za ukombozi wa elimu tumizi. Mwanga ni kukomboka kwa elimu tumizi.

Harakati hizi za kukomboa ukuzaji wa uongofu zinaendelezwa kupitia kwa jazanda ifuatayo: "Je, mti ukionyesha dalili ya kuoza, hukatwa matawi au hung'olewa mizizi?" (*Dunia Yao*, uk. 53).

Jazanda hii inahoji kuhusu suluhisho la kudumu dhidi ya tatizo la utandawazi unaokandamiza elimu tumizi ambayo inarejelewa kama mti na kudidimia kwake kama dalili za kuoza. Inakusudia kuhimiza ukombozi wa ukuzaji wa uongofu uliokandamizwa na utandawazi, dhana inayorejelewa kama kun'golewa mizizi katika dondoo. Wahusika mbalimbali wana maoni tofauti kuhusu suala hili lakini yote yameelekea kuhimiza ukombozi. Mhusika Sadiki anasema kuwa hakuna mashoka siku hizi kwa maana ya kuwa katika karne ya ishirini na moja uongofu haupo. Mhusika Kiwi anajibu mti unahitaji upogolewe matawi, lakini mikono iko mbali. Juma anasema unyunyiziwe dawa ya kuua magugu na wadudu lakini hamna pesa za kununulia. Mdungi anapendekeza ukatwe kwa ushirikiano wa watu wengi lakini kwa bahati mbaya watu wote ni vivuli hawana nguvu za kuukata. Bakari anang'ang'ania uchimbwe kwa ndole ung'olewe mizizi yote, usibaki hata mmoja, lakini ndole zataka mikono, tena imara. Anaendelea kuuliza kama watu wote wamekuwa vivuli tu, mikono na vidole vitatoka wapi? Majibu ya wahusika hawa wote ni utundikaji wa kijazanda unaolenga jambo moja; ukombozi wa elimu tumizi utakaowashirikisha Waafrika wote ili uongofu katika jamii uwe imara.

Kupitia kwa mhusika Ndumi katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, kuna ukombozi wa elimu tumizi iliyojengwa katika msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika jambo ambalo lilikuwa limevurugwa na utandawazi. Ndumi anaposhawishiwa na mamake achangamkie mafunzo yaliyoegemea zaidi kwenye utandawazi kuliko maarifa asilia ya Kiafrika huko shuleni kwao, Ndumi anadinda kama akisiko la ukombozi wa ukuzaji wa uongofu. Anasema kuwa:

> *"…hizo gymnastics wanakozifanya wanaanza watoto wakiwa umri mdogo sana na mambo ya skating nayo, huku kwetu hata hiyo theluji hatuna…!" (Msimu wa Vipepeo* uk 144).

Huu ni utundikaji wa kijazanda unaokejeli upungufu wa kimaarifa walionao watoto na vijana Waafrika. Upungufu huu ni zao la utandawazi ambao umewakosesha nafasi ya kupata elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika na yanayolenga kukuza uongofu. Ndumi anadhihirisha ukombozi kwa kupinga elimu ya kiutandawaz isiyozingatia kukuza uongofu. Badala yake anachangamkia kutafuta njia ya kuwasiliana na babake mzazi, Kalulu, na Kasoo, mfanyakazi wa nyumbani aliyefutwa kazi kwao nyumbani, ili afaidi masimulizi yao yanayosheheni uongofu. Mara kwa mara Ndumi anamfahamisha mamake,

Julia, kuhusu elimu yenye uongofu anayopokea kutoka kwa Kanda, babake mzazi. Kanda alikuwa na kipaji kikubwa cha kubuni visa na kuvisimulia. Mojawapo wa visa hivi ni hadithi inayomhusu nondo ambaye bila kutafakari aliuendea mwanga wa taa ya kibatari ambao hatimaye ulimwangamiza kwa kumchoma (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 112). Funzo kwa Ndumi kupitia kwenye hadithi hii ni kuwa awe mwenye kutafakari kabla ya kufanya uamuzi kwani yapo baadhi ya mambo yanayovutia katika mwonekano wa juu lakini hatima yake ni maangamizi.

Ndumi pia anafanikiwa kumshawishi mamake waende vijijini wakamtafute Kasoo na wamtafutie kazi. Ndumi anayafanya haya yote akiwa na nia ya kufaidi elimu yenye uongofu kutoka kwa Kasoo. Kabla ya Kasoo kufutwa kazi, msimulizi anasema kuwa alikuwa akimsimulia Ndumi hadithi nyingi za jamii yao na maarifa asilia ya jamii hiyo. Isitoshe kipindi hicho cha masimulizi alimpa Ndumi nafasi ya kujifunza kazi ya kufua nguo (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 73). Kwa hivyo kutokana na uchanganuzi katika sehemu hii, ni bayana kuwa elimu tumizi ikiimarishwa Mwafrika atajiletea maendeleo mwenyewe pasipo kutegemea misaada kutoka kwa nchi zilizoendelea. Sehemu ifuatayo tunaangazia namna vyombo vya kiteknohama vinavyoweza kuimarisha ufundishaji wa elimu tumizi barani Afrika.

## Jukumu la Wazazi Kutiliwa Nguvu na Vyombo vya Kiteknohama

Katika sehemu iliyotangulia, tulidhihirisha kuwa riwaya tulizozichanganua zinasawiri athari hasi za kuviachia vyombo vya kiteknohama jukumu la wazazi katika elimu tumizi. Katika sehemu hii, tunachanganua mtazamo mwingine zinaotutazamisha riwaya tulizozichanganua kuhusu vyombo vya kiteknohama. Mtazamo huu unapendekeza kuwa hata katika kipindi hiki cha utandawazi, wazazi wanafaa kuhakikisha kuwa wanatekeleze jukumu lao la kuwalea watoto katika malezi yanazozingatia elimu tumizi. Hawafai kuviachia vyombo vya kiteknohama jukumu hili bali wavitumie kufanikisha jukumu lao.

Hata katika kipindi cha utandawazi, mhusika Kanda, katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* bado ni imara katika elimu tumizi. Hili linabainika aliposhinikizwa na mpwa wake ajifundishe maarifa ya kutumia tarakilishi. Alikubali shinikizo hilo akiwa na nia ya kutumia ujuzi wa kiteknohama kuendeleza elimu tumizi kama inavyodhirika katika dondoo hii:

"Tangu siku alipopokea barua pepe ya kwanza, Kanda aliamua jambo moja- kuwa katika barua zake ataifanya kazi ambayo aliipenda sana alipokuwa akiishi na binti yake: kusimulia hadithi" (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 98)

Katika dondoo hii, mhusika Kanda anatumia chombo cha kiteknohama, tarakilishi, kuwasiliana na binti yake, Ndumi, ambaye hawakuwa wamewasiliana tangu kutalikiana na mkewe, Julia. Julia na Mkurutu wameviachia huru vyombo vya kiteknohama kuyaendesha malezi na elimu ya Ndumi kutokana na kasumba za kiutandawazi. Kwa upande wake Kanda, anavitumia vyombo hivi kama nyenzo tu za kufanikisha jukumu lake kama mzazi, la kuirithisha elimu tumizi kwa mwanawe kupitia kwa masimulizi. Ndumi anayakumbuka maneno yafuatayo aliyoyasoma kwenye barua pepe aliyotumiwa na Kanda:

> *"Tunazaliwa katika ukweli lakini tunaishi katika uongo. Kipepeo wangu, nitakueleza kwa nini. Mgogoro mkuu unaotokea katika maisha yetu huwa ni kati ya ukweli na uongo. Mgogoro huu ndio unaozaa ubaya na uzuri…drama kubwa ya maisha yetu inatokana na uono tunaouamini kujihusu sisi wenyewe. Uongo wa kwanza unaoamini unatokana na ile sauti inayokuambia: wewe si. Wewe si unavyopaswa kuwa; wewe si mzuri vya kutosha…Mwanangu, tunaanza kujisaka na kutafuta maoni kutoka kwa wengine…unanionaje? Nikoje? Ninavutia?"* (*Msimu wa Vipepeo*, uk. 152)

Masimulizi haya yanakusudia kumhimiza Ndumi ajithamini na asikubali kuathirika na matatizo ya kisaikolojia yanayotokana na kasumba za kiutandawazi zinazomdunisha Mwafrika na elimu yake tumizi. Hizi ni juhudi za kiukombozi. Aidha, mawazo haya yanatiliwa nguvu na mhimili wa kwanza wa nadharia ya utafiti katika Makala haya inayosisitiza kuwa kazi za sanaa zikusudie kumponya Mwafrika kutokana na matatizo ya kisaikolojia na udunishwaji kwa jumla.

Kutokana na juhudi hizi za Kanda za kuvitumia vyombo vya kiteknohama kumsimulia Ndumi hadithi, mtazamo wa Ndumi kuhusu elimu tumizi unakuwa wa kiukombozi. Ndumi anaanza kutofautiana na imani ya Mkurutu na Julia kuwa elimu tumizi yenye msingi katika maarifa asilia ya Kiafrika haina nafasi katika kipindi cha utandawazi. Ndumi anawapuuza Mkurutu na Julia kama walezi wake na kuonekana kuvutiwa na malezi na elimu ya babake mzazi, Kanda. Hili linadhihirika pale ambapo mara kwa mara Ndumi anamnasihi Julia kwa kutumia nasaha anazozipokea kutoka kwa Kanda kila Julia anapokabiliwa na changamoto. Ndumi pia anasawiriwa kama anayependa kupindukia kumwandama Kasoo ambaye ni kijakazi wa kwao nyumbani mwenye umri wa kuwa nyanyake ili afaidi hadithi za Kasoo kuhusu jamii yao; hadithi za zamani ambazo zilikuwa na mvuto wa aina yake. Mvuto huu ulitokana na kuwepo kwa elimu tumizi kwenye hadithi hizo iliyohusu mustakabali thabiti wa maisha ya kijana wa kike na ujifunzaji wa kazi za unyumba kama vile kufua nguo.

Mtazamo huu wa Ndumi wa kiukumbozi unashadidia madai ya mhimili wa pili wa nadharia ya utafiti katika makala haya kuwa Mwafrika mwenye elimu tumizi yenye msingi wa Kiafrika anafaa kuhimiza usawa wa watu wote bila kubagua. Hii ndio maana Ndumi anatofautiana na Mkurutu na Julia kuhusu umuhimu wa kusikiza masimulizi kutoka kwa wafanyakazi wa kwao nyumbani ambao sio matajiri kama wao. Licha ya kukatazwa kuwa na uhusiano wa karibu na wafanyakazi hawa, Ndumi anazidi kuwa na ukuruba nao na kuongoka kutokana na masimulizi yao yanayoelekea kuhimiza kupunguzwa na hatimaye kuondolewa kwa mipaka ya kitabaka katika jamii.

## HITIMISHO

Riwaya za *Dunia Yao*, *Msimu wa Vipepeo* na *Nakuruto* zinajikita katika suala moja kuu. Suala hili ni kupendekeza kuwepo kwa mustakabali mpya unaozingatia nafasi ya maarifa asilia ya Kiafrika kwenye elimu tumizi katika kipindi cha utandawazi ili kuikomboa elimu tumizi barani Afrika dhidi ya athari hasi za utandawazi. Suala hili kuu limebainika wazi kupitia mitazamo miwili mikuu. Kwanza ni athari za utandawazi kwa elimu tumizi ambazo zimedhihirika kwenye dhamira ndogondogo kama vile: dhana potofu kuhusu elimu tumizi yenye msingi wa maarifa asilia ya Kiafrika, kupuuzwa kwa elimu tumizi katika ukuzaji wa uongofu na jukumu la wazazi kutwaliwa na vyombo vya kiteknohama. Pili ni ukombozi wa elimu tumizi dhidi ya utandawazi ambao umedhihirishwa na dhamira ndogondogo zifuatazo: mustakabali mpya kwenye elimu tumizi barani Afrika, kuhimiza elimu tumizi katika ukuzaji wa uongofu na jukumu la wazazi kutiliwa nguvu na vyombo vya kiteknohama. Dhamira hizi zinafafanua uelewaji wa changamoto zinazokumba elimu tumizi barani Afrika katika kipindi utandawazi na kupendekeza hatua za kusuluhisha changamoto hizo. Kimsingi linalosisitizwa na kazi hizi za kifasihi ni kwamba Mwafrika hana budi kuikomboa kuimarisha na kuendeleza elimu tumizi yenye msingi katika maarifa asilia ya Kiafrika ilia pate maendeleo thabiti. Elimu tumizi ni kigezo mwafaka cha kutathmini maendeleo barani Afrika katika kipindi cha utandawazi.

## MAREJELEO


Mbiti, J. (1989). *African Religions and Philosophy*. London: Heinemann.

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

Mokoena, K. (2017). *Black Aesthetics and the Son of Man Film*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Pretoria, Pretoria, Afrika Kusini).

Momanyi, C. (2009). *Nakuruto*. Nairobi: Longhorn.

Muppidi, H. (2004). *The Politics of the Global*. Minneapolis and London: University of Minnesota Press.

Murithi, J. J. (2017). *Itikadi Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*. Tasnifu ya uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. Imerejelewa kutoka http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/12314. (Tarehe 10/7/19).

Mwirabua, A. (2014). *Ukoloni Mamboleo na Utandawazi Katika Tamthilia Teule*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi,

Kenya. Imerejelea kutoka http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/12311

Nangoli C. M. (2002). *No More Lies About Africa*. East Orange: N.J:A.H.

Nkonge, E. (2014). *Ujumi Mweusi Katika Tamthilia za Nitaolewa Nikipenda na Mukwava wa Uhehe*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. Imerejelewa kutoka http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/12314. (Tarehe 16/4/17).

Wa Thiong'o, N. (2009). *Re-membering Africa*. Nairobi: East African Educational Publisher.

Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2006). *Msimu wa Vipepeo*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.